

Maoni na Majibu kutoka kwa Wasomaji na Rafiki, Hadithi na Taarifa Nyingine...

Ujenzi wa Kanisa umesukumwa na milioni 4.1

## MICHANGO YA PARISH HARAMBEE 2014

by the Harambee Committee

Kamati ya Harambee, iliyokutana Jumatano 19 Machi, inatoa matokeo ya michango. Kwa jumla tumeweza kupata zaidi ya milioni 4.1!

Baba Paroko na Wanakamati wanashukuru sana Wakristu, Marafiki na Wageni, wafanyakazi na wote walioshiriki ili Harambee ifaulu.

<b>CASH</b>	Before Harambee	<b>36,100</b>	
	On Harambee Day	870,600	
	After Harambee	35,700	
	<b>TOTAL</b>		<b>942,460</b>
<b>BANK / CHEQUES</b>	<b>TOTAL</b>		<b>430,000</b>
<b>M-PESA</b>	<b>TOTAL</b>		<b>121,150</b>
<b>LOCAL CHURCHES before Harambee</b> <i>(see details here below)</i>	Maize	295,563	
	Iron-sheets	495,860	
	<b>TOTAL</b>		<b>791,423</b>
<b>FRIENDS from Venice</b>	Bells	1,500,000	
	Building	360,000	
	<b>TOTAL</b>		<b>1,860,000</b>
<b>GRAND TOTAL</b>			<b>4,145,033</b>

### Details of Contributions from the Local Churches before Harambee

Local Church	MAIZE		IRON-SHEETS	
	Bags	Value @ 2500	Done	Balance
Kabati	15 bags	37,500	40,800	35,200
Mithuri	8 bags + 45 kg	21,251	46,040	20,460
Minjore	19 bags + 58kg	49,112	53,900	3,100
Githima	24 bags + 60kg	61,668	56,220	19,780
Gitwamba	1bag + 3kg	2,583	5,150	4,350
OI Motunyi	-	-	4,000	5,500
Kahuho	40kg	1,112	28,500	0
Mbombo	-	-	19,700	8,800
OI Moran	24 bags + 39kg	61,084	129,850	(+6,350)
Miharati	9 bags	22,500	29,400	(+900)
Survey	6 bags + 45kg	16,251	19,000	0
Magadi	6 bags + 68kg	16,890	21,850	6,650
Mouarak	-	-	3,600	15,400
Ngare Narok	-	-	9,100	9,900
Nagum	47kg	1,306	6,900	12,100
Dam Mbili	64kg	1,779	-	19,000
Lounyek	-	-	2,700	16,300
OI Donyo Ariwo	1 bag	2,500	13,450	5,550
C.A.	-	-	700	-
Friends	-	-	5,000	90,000
<b>TOTAL</b>	<b>118b&amp;19kg</b>	<b>295,563</b>	<b>495,860</b>	<b>264,140</b>

## Wageni na Marafiki wa Harambee

Wageni na Marafiki waliohudhuria Harambee:

### - Makanisa

Mons. Luigi Paiaro, Askofu Mstaafu wa Jimbo la Nyahururu na Mgeni Mkuu wa Harambee; Rev. Samuel Kariuki na Rev. Rose (ACK OI Moran).

### - Wanasiasa na Serikali

Hon. Jane Apollos (Laikipia Women Rep.) & Dr. Apollos (Egerton University); Hon. J.B. Akaale (County Minister for Education), representing His. Ex. The Governor J. Irungu; Hon. Jacob E. Endom (MCA Sosian, Laikipia); Hon. Peter Thomi Waigwa (MCA Githiga, Laikipia); Hon. Dan Ndegwa Macharia (MCA OI Moran Ward); Hon. Ann Cheptoo (County Minister for Sport & Gender); Mr. Fred Muganda (OCS OI Moran); Mr. Dickson Oseko; Inspector Kingori (AP).

### - Wafanyabiashara

Mrs. Monicah Kailemia (OI Moran); Mr. Kainamia (Kinamba); Sammy Ndungu (Total Petrol Station, Kinamba); Luke Kigen (Petrol Station, OI Moran); Mr. Philip Ndegwa (OI Moran); Mr. Lotich (OI Donyo Ariwo).

### - Marafiki

Peter Muchiri Ikinya (KNH Nairobi); Mrs. Catherine Waigwa & Mr. Samuel Githu (Nairobi); Mrs. Kuki Gallmann (Laikipia Nature Conservancy); Mr. Stephen Ali Apetel (Laikipia Nature Conservancy); Mr. Peter Githinji (Kenya Scouts Association); Mr. John Mwangi (Munyaka Sec. Sch.); Mr. Robert Kamau & Mrs. (ROBKAM) Mr. Joseph Njuguna & Mrs. (ROBKAM); Mr. George Mbugua (Sipili Mat. & Nursing Home); Ms. Teresa Wanjah (OI Moran); Mr. J. Kirabi (OI Moran Pry.); Mr. Joseph Murega (St. Martin CSA, Nyahururu); Mr. Murage (CDF Nyahururu); Mr. Dominic Ndegwa (OI Moran); Mrs. Margaret Maina (Mithuri Sec. Sch.); Mr. P.K. (Lariak Pry.); Tumaini Academy; Hekima House; YCS OI Moran Sec. School.

### - Marafiki kutoka Ng'ambo

Arch. Stefano Battaglia (Venice, Italy) Fr. Fausto Bonini (Venice, Italy); Fr. Silvano Bellomo (Paris, France); Mr. Roberto Solinas (Sassari, Italy).

### Baadhi ya Wageni waliotuchangia bila kuweza kuhudhuria:

Rt. Rev. Bishop Joseph Mbatia (Nyahururu); Rt. Rev. Bishop Kihara (Marsabit); Rev. Fr. Joseph Waititu (Nyahururu); Rev. Fr. Paul Maina (Maralal); Rev. Fr. Sandro Ferretto (Mochongoi); Rev. Fr. Vittorio Grigoletto (Weru); Rev. Fr. Mariano Dal Ponte & St. Martin CSA Community (Nyahururu); Mr. Richard Wachira (Maralal); Mrs. I.N. Wamithi (Nyahururu); Hon. GG Kariuki; Hon. Agnes Keshine (Minister for Security, Laikipia County); ; Mrs. Anita (Padua, Italy); Mr. Lomoe (OI Moran); Mr. William Wamungunda (Garage, Nyahururu); Mr. J. Njuguna (Survey); Mr. Mwaniki (Kitale); Mr. D.K. Kimiti (OI Moran Sec. Sch.); Mr. Laban Koech (OI Moran Sec. Sch.); Mr. Francis Gatimu (Mirango Pry.); Pst. James Mbuni (Naivasha); Mr. W. Kimani (Shining Star, Sipili); Mr. Gitahi Kihuto (Sipili); Mr. Waweru (Wizara ya Maji); Mr. E. Omondi (E.O. OI Moran); Mr. R. Wanjohi; Mr. J. Wanderi; Mr. Linus Maina; Mr. Luke Wambugu; Mr. Peter Nyamu; Mr. J. Ngugi (Mukuyu M-Pesa); Spear Supermarket (Nyahururu); Nyahururu Hardware; Mr. Titus Muia (NSSF); PCEA OI Moran; Deliverance Church OI Moran; Pst. Wachira (Deliverance Kinamba); AIC Survey; Ms. Mary A. Ndegwa; Lounyek Pry; Ms. Esther Njenga.

Hapa hayajaandikwa majina ya Wakristu wa makanisa yetu, bali hasa majina ya Wageni na Marafiki.

Tuwie radhi ikiwa yamesahulika majina mengine.

To All Friends, Guests, Well-Wishers & our Christians

SAINT MARK CATHOLIC PARISH - OI Moran

## THANK YOU

For your Support and for your Friendship.

Be blessed!

**Kwa Marafiki na Wafadhili ambao hawajaweza kuchangia mradi wa Kanisa: bado kuna nafasi! Kazi ya ujenzi haijakwisha. Karibuni!**

### Mchango wa KUNI kutoka Local Churches

- Parokia inaendelea kukusanya kiasi cha kuni kutoka katika kila kanisa, kufuatana na mpango wa mchango huu uliotolewa mwezi uliopita.
- Wakristu walete kuni nzuri katika kanisa lao.
- Viongozi wamjulisha bw. Joseph Kariuki wakiwa tayari na michango ya kanisa lao
- Siku ya mwisho tayari imepita (Mwisho wa Februari). Mkanisa ambayo hayajamaliza yajaribu kuharakisha.

### Suala Nyeti

## KANISA LAJENGWA NA KINA NANI?

by Mr. Peterson Muthua Wangeci,  
from U.K. – United Kabati

OI Moran ni sehemu ambayo kwa miaka mingi watu wameitaja kama mahali ambapo hakuna usalama: na si uongo, usalama mara nyingi unakosa. Sawa!

Wengi wametaja kama mahali ambapo hapana chakula, **excuse us please**, OI Moran kuna chakula kingi, mahindi, maharagwe, **Water Melon na Sweet Melon**, Pili-Pili Hoho, Nyanya na kadhalika... Pia wasema ni mahali ambapo pana umaskini si haba... Haya yote ni madai ya wale hawana ufahamu kutuhusu.

Tukisoma katika kitabu kitakatifu cha Biblia, kuna wakati watu waliposikia Yesu akisifiwa jinsi anavyofanya kazi, kufanya miujiza, kuponya magonjwa, kufufua wafu na kusamahe dhambi, kuna wale ambao walishidwa kujua ni kitu gani kizuri kiwezacho kutoka Nazareti. Hawakuamini Nazareti kijiji kidogo kinaweza toa Nabii, Daktari na kadhalika. Kama vile Nazareti, hata OI Moran kuna watu watajiuliza, nini inaweza kutoka OI Moran! Watu wa nje ambao hawajui ukarimu wa watu wa OI Moran, huwaona wenyeji wa hapa kama watu wasio na mbele wala nyuma.

Watu wa OI Moran ni watu ambao labda hawana pesa nyingi, lakini wana roho za ukarimu, na hii ndiyo sababu inanibidi kurudia mithali ambayo nilisikia siku moja:

**“Kanisa hujengwa na pesa za maskini, mabaki ya matajiri, na machozi ya Baba Paroko!”**

Jambo hili lilidhihirika wazi siku ya Jumapili tarehe 9/3/2014, siku wakristu na wenyeji wa OI Moran, wakisaidiwa na marafiki, walijitokeza kuchanga pesa za kumaliza ujenzi wa Kanisa, kazi ambayo ilianza yapata miaka mitatu iliyoisha, tulipofanya Harambee ya kwanza mnamo Jumapili tarehe 27/11/2011, tukisaidiwa na mwenda zake Hayati George Saitoti, Mungu airehemu roho yake. **It was not business as usual**, kila mtu alikuwa ngangari kwa mchango huu, **and the best thing this time**, hakukuwa na siasa chafu kama vile tumezoea katika mikutano mingi ya kuchanga pesa.

**Well**, labda hatuwezi kukosa mmoja na kitendawili cha makamasi, lakini hayo ni macho ya chura ambayo daima dawamu hayatamzuia ng’ombe kunywa maji. Watu walikuwa na nidhamu ya kutosha, wakaonyesha ukarimu, **with utmost God faith**. Pia, najua kuna watu walikuwa na matarajio makubwa kuhusu ni nani angetoa nyingi na ni nani angetoa kidogo. Lakini mithali huenda, usinione mdogo ukanidharau, mimi naweza fanya maajabu, na hii ikadhihirika wazi wakati watu waliamka kutoa pesa. Walio wadogo wakatoa zaidi ya wengine wengi!

Pia, kazi ya watu wetu. Wanakwaya walitoa sauti kama ninga kufanikisha ibada ya Misa, nazo burudani zilitolewa kwa mihemko, kutoka kwa **OI Moran Peace Club**, Wanafunzi wa shule ya Mchungaji Mwema Maralal, bila kuwasahau Watoto wa Tumaini.

Makala haya yangependa yakutoa shukrani zetu kwa watu wa OI Moran na marafiki, ambao walitoa pesa zao kwa ukarimu na kisha zikajaza kibaba, chambilecho wahenga haba na haba..., watu wa class wanimalizie. Hujaza kibaba. Tunge-taka pia kutoa shukrani zetu za dhati kwa watu ambao walifanya kazi ambayo kwa wengi iliyonekana ya kawaida, kwana ni wakurungezi ama **managers** wa Simba Kiosk wakiongozwa na Bw. Anthony Njogu ambaye ndiye alikuwa **C.E.O.**; Bw. Derrick Gitahi Wanjiru ambaye alikuwa afisa wa usalama yaani **Security Officer**; Bi. Fidelis Wangui Wanjiku **Sales manager** na Bw. Abdinoor afisa wa uhusiano wa umma yaani **Public Relation Officer**. Hawa ni wale ambao walihakikisha kuwa bwana-tumbo amepata chakula. Chips zilipikwa kama za fujo, usafi ulihakikishwa na wangwana wakashiba. Vijana wa Parokia na wanafunzi wa Hekima House pia walihakikisha pesa zimepatikana, wakiuza maua kwa wingi lakini kwa bei ya kila mtu.


Ama kwa hakika, kanisa linajengwa na pesa za maskini, mabaki ya matajiri na machozi ya **Parish Priest**, lakini kwangu, hili ni Suala nyeti!

### Maisha ya Kanisa na Ushuhuda wa Watakatifu

## ST. JOHN PAUL II & ST. JOHN XXIII

**Jumapili 27 Aprili, Roma, katika ibada ya Misa ya Jumapili ya pili ya Paska, Papa Fransisko atatangaza rasmi Papa Yohane Paulo wa 2 na Papa Yohane wa 23 kuwa Watakatifu.**

- **John Paul II** (Karol Wojtyla, from Poland) was the Pope for 27 years, from 16.10.1978 to 2.4.2005. He led the Church through many challenges of the last Century, visiting almost all countries in the world; he introduced the Church into the Third Millennium.



- **John XXIII** (Angelo Giuseppe Roncalli, from Italy), was the Pope for 5 years, from 28.10.1958 to 3.6.1963. During his Pontificate he announced and opened the Second Vatican Council and worked hard for promoting peace among nations.